

Uvimbe wa Misuli ya Moyo baada ya Chanjo ya COVID-19: Yale Ambayo Wazazi na Watu Wazima Wadogo Wanafaa Kujua



Uvimbe wa misuli ya moyo ni nini?

Uvimbe wa misuli ya moyo (na uvimbe) ni istilahi za kufafanua uvimbe ndani ya au katima moyo. Dalili za kawaida zinajumuisha maumivu ya kifua, ugumu wa kupumua, na kuhisi kana kwamba moyo wako unadunda mbio sana. Mfumo wa kingamwili wa mwili mara kwa mara unaweza kusababisha uvimbe huu katika kuitikia maambukizo, kama vile virusi.

Uvimbe wa misuli ya moyo si kawaida sana na huwa hauna madhara sana.

Kuna chini ya visa 200,000 vya uvimbe wa misuli ya moyo Marekani kila mwaka, vikiwa na chini ya 2% ya kuwa na madhara. Hakujakuwa na vifo kutokana na uvimbe wa misuli ya moyo vilivyojitlea kusababishwa na chanjo ya COVID-19 Marekani.



- Haijulikani kuwa inaweza kusambazwa
- Visa vingi ni vya chini
- Matibabu kila mara huwa ya chini, yanayolenga kudhibiti dalili

Je, kuna muunganisho wowote na chanjo ya COVID-19?

Inawezekana. Hatari ya baada ya chanjo ni nadra sana, lakini inaweza kufanyika. Uvimbe wa misuli ya moyo pia hutokea kwa watu ambao hawajapokea chanjo.

Kwa sababu haiwezi kupuuzwa, jopo la usalama la Centers for Disease Control and Prevention (CDC, Vituo vya Udhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa) limebainisha kuwa kuna "muungano unaowezekana" kati ya uvimbe wa misuli ya moyo na chanjo za COVID-19 za mRNA (zilizoundwa na Moderna na Pfizer-BioNTech).

Nafaa kufahamu dalili na ishara zipi baada ya chanjo?

Visa vimetokea sana katika wavulana na wanaume wadogo wenye umri wa chini ya miaka 30. Dalili zinaonekana kuwa za kawaida zaidi baada ya dozi ya pili.

CDC inapendekeza kuwa watu waliopewa chanjo hivi karibuni watafute matibabu wakiwa na dalili yoyote kati ya hizi baada ya kupokea chanjo, hasa katika wiki ya kwanza baada ya chanjo:



- Maumivu ya kifua
- Upungufu wa pumzi
- Hisia za kuwa na moyo unaodunda haraka, ulio sawasawa au moyo unaoonga

Nafasi ya haya kutokea ni nadra sana. Hata hivyo, tafuta usaidizi wa kimatibabu mara moja ukipitia yoyote kati ya dalili hizi.

Kumbuka, ni kawaida kuwa na dalili za chini hadi za wastani, ikijumuisha homa, maumivu ya kichwa, uchovu, na maumivu ya kiungo/misuli, wakati wa wiki ya kwanza baada ya kupokea chanjo yoyote ya COVID-19 Madhara haya mara nyingi yanafaa kuanza ndani ya siku tatu baada ya kupata chanjo na yanafaa kukaa tu kwa siku chache.

Chanjo bado ni chaguo bora zaidi

Manufaa thabiti za chanjo yanashinda kwa umbali hatari ya chini ya uvimbe wa moyo. Chanjo inafanya kazi vizuri sana katika kuzuia kifo na ugonjwa, na inajumuisha ulinzi dhidi ya aina za virusi mpya na hatari zaidi.



DOH 348-835 August 2021 Swahili

Ili kuomba waraka huu katika muundo mwingine, piga simu 1-800-525-0127. Wateja amba ni viziwi au wasio na uwezo wa kuzungumza, tafadhali piga simu 711 ([Washington Relay](mailto:civil.rights@doh.wa.gov)) au tuma barua pepe civil.rights@doh.wa.gov.